

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI



TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI.

Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni leo jumanne tarehe 06/03/2018 ,katika Mkutano wake maalumu wa Baraza la Madiwani limepitia na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kawaida na mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2018/2019 ambapo Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inatarajia kukusanya /kupokea kiasi cha **Tshs 242,185,292,987.00** ambapo **Tshs 209,436,308,079.00** sawa na **86.5** ni Ruzuku kutoka Serikali Kuu, **Tshs. 686,380,000.00** sawa na **0.3%** ni mchango wa Jamii na **Tshs.32,062,704,908.00** sawa na **13.2%** ni Mapato ya ndani ya Manispaa.

Kati ya fedha hizo zilizopitishwa,kiasi cha **Tshs 120,326,705,873.00** ni Matumizi ya Kawaida ambayo ni sawa na asilimia **49.7** ya bajet yote na **Tshs.121,858,587,114.00** ni Fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo ni sawa na asilimia **50.3** ya bajeti.

Aidha katika Fedha hizo Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inatarajia kukusanya kiasi cha **Tshs 32,749,084,908.00** kutoka vyanzo vyake vya ndani ambapo **Tshs 16,392,166,400.00** zitatumika kwa matumizi ya kawaida na **Tshs.16,356,913,508.00** zitatumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo ,na Fedha za Ruzuku kutoka Serikali Kuu, ni **Tshs. 209,436,208,079.00** zitakazojumuisha kiasi cha **Tshs 103,934,539,473.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Tshs. 105,501,668,606.00** kwa ajili ya Miradi ya maendeleo.

Mishahara ya watumishi, kutokana na mapato ya ndani ni **Tshs.906,498,855.00** na Mishahara kutokana na ruzuku ya Serikali kuu ni **Tshs.99,590,270,811.00**, na

kufanya jumla ya Tshs. 100,496,769,666.00. Fedha kwa matumizi mengineyo ni Tshs, 15,485,667,545.00 kutoka vyanzo vya ndani na


Tshs. 4,344,268,662.00 kutoka ruzuku ya serikali kuu na kufanya jumla ya matumizi mengineyo kuwa Tshs, 19, 829,936,207.00.

Kwa mujibu wa Taratibu za Kibajeti mpango huu umeandaliwa kwa kuzingatia Sera na Miongozo ya Kitaifa, Sheria ya Bajeti Na.11 ya mwaka 2015, Dira ya Taifa nya Maendeleo ya 2025, Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe, John Pombe Joseph Magufuli tarehe 20/11/2015 ,Malengo ya maendeleo endelevu ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020 , Mpango wa tekeleza kwa Matokeo Makubwa sasa (BRN), Sera ya Taifa ya UKIMWI, Sera za Kisekta, Mpango Shirikishi Jamii ya Fursa na Vikwazo kwa maendeleo (O&OD) ya Kata na Mitaa na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa sura ya 290 iliyofanyiwa marekebisha mwaka 2010 .

Maeneo yaliyopewa kipaumbele katika mpango huu ni pamoja na kuboresha na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Manispaa,kuboresha miundombinu ya kiafya , shule za msingi na Sekondari,kuboresha miundombinu ya maji barabara na kilimo mijini,kuboresha hifadhi ya mazingira na ukusanyaji wa Taka, kuimarisha ushirikishaji wa jamii katika upangaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo,na kuboresha mazingira ya wafanyabiashara wadogowadogo.

Ili kufikia Mafanikio yaliyokusudiwa Halmashauri ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni itaimarisha mahusiano mazuri kati ya Serikali, Mashirika yasiyo ya Kiserikali,na wadau wengine, itaendelea kujenga uwezo na ujuzi kwa watumishi katika utoaji wa huduma zilizobora na za Haraka,itaimarisha utawala bora uwajibikaji na uwazi na kujenga uwezo kwa viongozi wakiwemo waheshimiwa madiwani,na wenyeviti wa Serikali za Mitaa katika kusimamia shughuli za wananchi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni.

Aidha Mpango wa Matumizi na bajeti ya mwaka 2018/2019 ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020. Hivyo matokeo ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti hii yameelekezwa katika kujibu matarajio ya watu ambayo ni utatuzi wa kero zao pamoja na maisha bora kwa kila Mtanzania.



Sebastian M. Mhowera

**AFISA UHUSIANO WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI.**